**Difasi Idude Isabirye, (1929–2013)**

Difasi Idude Isabirye alikuwa mchungaji na msimamizi nchini Uganda na Kenya. Kujitoa kwa Isabirye kwa uongozi wa kanisa kulionyeshwa zaidi wakati wa siku ngumu za utawala dhalimu nchini Uganda katika miaka ya 1970.

**Maisha ya Awali**

Difasi Isabirye, kutoka kabila la Musoga, alizaliwa na Fenekansi Idude na Robina Kafuko mnamo Juni 15, 1929, katika kijiji cha Butale, kata ndogo ya Bugulumbya, wilaya ya Kamuli, Mashariki mwa Uganda. Alikuwa mdogo kati ya wana wawili na watoto wa pekee wa wazazi wao. Ingawa baba yake alikuwa na wake wawili, mke mwingine hakuwa na watoto. Yeye na Sofatiya kaka yake walikua wakichunga mifugo ya baba yao, ambayo ilikuwa kazi ya wavulana wote kijijini zamani hizo. Difasi alisoma shule ya msingi ya Nawanende SDA ambapo alijiunga na Kanisa la Waadventista Wasabato kwa ubatizo mwaka 1945. Kutoka Nawanende aliendelea na masomo hadi Chuo cha Ualimu cha Nchwanga katika wilaya ya sasa ya Kakumiro, Uganda Magharibi. Nchwanga kilikuwa kituo cha kwanza cha Waadventista Wasabato nchini Uganda, ambacho kilianzishwa mwaka 1927 na SG Maxwell, Muingereza, na Petro Risase, Mtanzania.

**Uongofu na Ndoa**

Mnamo mwaka wa 1941 Kanisa la Waadventista Wasabato lilifanya mkutano wa injili huko Nawanende, mkutano ambao ulifanikiwa sana. Ingawa hawakuwa makini na kanisa, wazazi wa Difasi walijiona kuwa washiriki wa Kanisa la Uganda (Anglikana) na walitarajia watoto wao wawe hivyo. Kwa sababu hiyo Baba yake Difasi aliwaambia watoto wake wasiende kwenye mikutano ya Waadventista Wasabato. Kama ilivyo desturi ya watoto wengi wa Kiafrika kutii wazazi wao, hasa katika siku hizo, wavulana walilazimika kutii. Hata hivyo, baba yake alitaka Difasi awe mwalimu wa kilimo, na kwa sababu hiyo, mwaka 1943, alimruhusu kusoma Shule ya Msingi ya Waadventista ya Nawanende, ambayo ndiyo tu ilikuwa imeanzishwa, ili aweze kuweka msingi wa kuwa kile alichotaka kuwa. Difasi anasimulia, “Nikiwa shuleni, nilikutana ana kwa ana na njia tofauti kabisa ya maisha. Nilijiunga na shule niliyohisi zaidi kama familia kubwa; familia ambapo kila mshiriki alitunzwa, na Kristo aliruhusiwa katika maisha ya wanafunzi na walimu kwa njia ya ajabu na ya maana. Hakika, ilikuwa wakati nikiwa katika shule hii ambapo Kristo alikuja kuwa ukweli kwangu, si dhana dhahania kama Alivyokuwa nilipokuwa nikichanganyika na jumuiya ya Kianglikana.”

Mnamo 1944, wakati wa juma la maombi, Difasi alichukua msimamo wa kuwa upande wa Yesu, lakini kwa kumwogopa baba yake, hakujitoa kubatizwa. Ubatizo ulikuja mwaka mmoja baadaye alipoamua kubatizwa tarehe 5 Desemba 1945 akibatizwa na Mchungaji M. Kabala. Kama ilivyotarajiwa, baba yake, aliposikia juu ya ubatizo wake, alimfukuza kutoka nyumbani kwake, na alirudi tu baada ya siku chache baada ya uingiliaji kati wa mama yake, ambaye alikuwa amemshinda mumewe kwa ushawishi.

Akiwa mwanafunzi wa Nawanende, alikutana na msichana mdogo, Ruth Zewulensi, aliyezaliwa Desemba 24, 1937. Binti huyu mdogo wa Musoga aliyemvutia hatimaye akawa mke wake Januari 24, 1952, huko Nawanende. Wakati wa ndoa yao, alikuwa mfanyakazi huko Nchwanga, ambako aliwekwa kama mwalimu mafunzoni. Difasi na Ruth walibarikiwa kupata watoto wanne; yaani, David Isabirye, Samuel Isabirye, Joyce Isabirye, na Stephen Isabirye.

**Elimu na Uchungaji**

Mnamo 1953 Isabirye alihudhuria kozi ya huduma ya miaka miwili katika Chuo cha Misheni cha Bugema, kozi iliyoendeshwa na mmishonari wa Uingereza, Mchungaji Conrad Hyde, na Mchungaji wa Uganda Yekoyada Bamanya.

Kozi hiyo ilikuwa ya watu ambao hawakuwa na cheti cha kiwango cha kawaida (shule ya sekondari). Ilikuwa ni kwa sababu hii kwamba baada ya kuhudumu katika kanisa la Uganda kama itakavyoonyeshwa, alirejea shuleni na kumaliza kozi ya cheti cha shule ya sekondari (O-Level) katika Chuo cha Misheni Bugema mwaka 1965. Mwaka 1968-1971 aliendelea na masomo ya shahada ya kwanza ya dini katika Chuo cha Solusi (sasa ni chuo kikuu) huko Rhodesia ya Kusini (sasa Zimbabwe). Mnamo 1981 na 1982 alichukua digrii ya uzamili katika dini katika Seminari ya Mashariki ya Mbali huko Ufilipino, na kupata digrii hiyo mnamo 1982.

Difasi Isabirye alijiunga na huduma ya kanisa kwa mara ya kwanza mwaka wa 1951 kama mwalimu/mwinjilisti huko Nawanende, Mashariki mwa Uganda. Mnamo 1952 alifanya kazi kama mwalimu/mwinjilisti huko Nchwanga. Mwaka uliofuata alijiunga na Chuo cha Misheni cha Bugema kwa kozi ya huduma ya miaka miwili, na ilipokamilika alitumwa katika Mtaa wa Kanisa la Nsube Mashariki mwa Uganda kama mwinjilisti. Kati ya 1957 na 1967 alikuwa mkurugenzi wa uchapishaji na msimamizi wa idara ya Sauti ya Unabii. Ilikuwa katika kipindi hiki ambapo alitawazwa kuwa mchungaji wa Kanisa la Waadventista Wasabato mnamo Septemba 1960 katika Kanisa la SDA la Najjanankumbi huko Kampala.

Mnamo 1972 alikuwa mkurugenzi wa Kituo cha Misheni cha Rwenzori huko Fort Portal, Magharibi mwa Uganda. Mwaka 1973 –1979 aliwahi kuwa mkurugenzi mkuu na (rais) wa Uganda Mission Field. Hiki kilikuwa kipindi kigumu sana kwa kanisa. Mtangulizi wake, Robert Carter (raia wa Marekani) alikuwa ametangazwa kuwa mtu asiyefaa na ghafla alirejea katika nchi yake kwa kuwa alikuwa Mmarekani ambaye Idi Amin alikosana naye na akapewa saa 72 ya kuondoka.

Mwaka 1980–1981 alikuwa mkurugenzi wa Sauti ya Unabii makao makuu ya Umoja wa Afrika Mashariki yenye makao yake makuu Nairobi, Kenya. Ofisi yake ilikuwa Karura ambako Sauti ya Unabii ilikuwa na makao yake. Mnamo 1982–1986 aliteuliwa kuwa mwalimu katika kozi ya wahudumu katika Shule ya Ualimu ya Kamagambo huko Kisii, Kenya. Aliondoka Kamagambo kuhudumu kwa mwaka mmoja (1987) kama mkurugenzi mtendaji wa Fildi ya Magharibi mwa Uganda. Mnamo 1988 – 1990 alikuwa

katibu mtendaji wa Union mpya iliyopangwa ya Uganda, iliyoundwa rasmi mnamo 1987 chini ya uongozi wa mmishonari wa Kiamerika Dk. Jack Bohannon. Mchungaji Isabirye alistaafu kutoka kwa huduma za kanisa mwaka wa 19919 na kurudi nyumbani kwake Kasambira, wilaya ya Kamuli, Mashariki mwa Uganda, si mbali na jiji la Jinja.

Alifariki Machi 19, 2013, na akazikwa nyumbani kwake Kasambira huko Busoga. Mkewe Ruth ambaye alikuwa mkono wake wa kulia katika huduma yake kwa karibu miaka hamsini pia alipumzika mnamo Julai 30, 2020, na alilazwa karibu na mumewe huko Kasambira.

**Urithi Aliotuachia**

Isabirye alikuwa msambazaji hodari wa uinjilisti wa vitabu nchini Uganda na Kenya, na aliwahimiza vijana wengi kufanya kazi kama wainjilisti wa vitabu.

Ahadi ya Isabirye kwa uongozi wa kanisa ilionyeshwa wakati wa siku ngumu za utawala wa Idi Amin Dada. Mnamo mwaka 1977 serikali ya Idi Amin ilitangaza kupiga marufuku madhehebu 27, ikiwemo na Kanisa la Waadventista Wasabato. Isabirye, akiwa kiongozi wa Kanisa la Waadventista nchini, hakutetereka bali alishauri waumini wa kanisa hilo kutokaidi agizo hilo na badala yake wafanye ibada zao majumbani mwao. Huu ulikuwa ushauri mzuri. Pamoja na aliyekuwa mweka hazina wa Uganda Mission Field, Sekikubo Sendawula, Isabirye alilinda fedha za kanisa kwa wivu mkubwa akihakikisha kwamba wafanyakazi wote katika kipindi cha marufuku hiyo wanapokea mishahara yao na posho zote wanazostahili. Chini ya usimamizi wake katika kipindi cha marufuku, taasisi na mali nyingi za Kanisa la SDA nchini (mbali na Hospitali ya Ishaka) zilibaki bila kuathiriwa na serikali hadi utawala wa Amin ulipoanguka Aprili, 1979. Mungu akiwa kiongozi wake, aliongoza kanisa kwa uthabiti na matumaini makubwa.